TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

TUME YA USHINDANI NA SHIRIKA LA VIWANGO (TBS) WAENDESHA UKAGUZI KATIKA VIWANDA VYA MABATI JIJINI DAR ES SALAAM

Taasisi tatu kati ya tano zinaozunda kikosi kazi mahsusi cha kukabiliana na bidhaa bandia (Anti-Counterfeit Task-force), Tume ya Ushindani, Shirika la Viwango Nchini (TBS) na Jeshi la Polisi, jana, Ijumaa, tarehe 22 Februari, 2013 ziliendesha zoezi la pamoja la ukaguzi wa viwanda viwili vinavyozalisha mabati jijini Dar es Salaam.

Viwanda hivyo ni KAMAKA kilichopo eneo la Buguruni, na Dragon Roofing Sheets kilichopo eneo la Vingunguti, jijini Dar es Salaam.

Ukaguzi huo umetokana na kuongezeka kwa malalamiko kutoka kwa wateja wa viwanda hivyo kuwa bidhaa zinazozalishwa na viwanda hivyo zimeonekana kutokidhi matarajio ya matumizi yake na hivyo kuamini kuwa hawapati thamani halisi ya fedha walizotumia katika kununua bidhaa hizo.

Katika ukaguzi huo Tume ya Ushindani kwa kushirikiana na maafisa kutoka TBS na Jeshi la polisi waliweza kubaini kwa ukiukwaji taratibu kadhaa za uzalishaji na usimamiaji wa ubora wa bidhaa katika kiwanda cha Dragon Roofing Sheets na kuwataka wazalishaji hao kuzingatia taratibu hizo.

Baadhi ya kasoro zilizojitokeza ni pamoja na:

1. Bidhaa za kiwanda hicho kutowekwa taarifa zozote za uzalishaji kama batch number, aina ya madini za kuzuia kutu zilizotumika katika kutengeneza bidhaa hizo na katika bidhaa za kiwanda hicho hakukuwa na nembo yoyote inayokihusisha kiwanda hicho na uzalishaji wa bidhaa husika. Kasoro hii inatoa mwanya kwa wafanyabiashra wasio waaminifu kuweza kutumia nembo za wazalishaji wengine wa bidhaa hizo na kuwafanya wateja kuamini kuwa zinatoka kwa wazalishaji ambao nembo zao zimeghushiwa. Aidha, kukosekana kwa taarifa za mzalishaji katika bidhaa kunawafanya watumiaji wa bidhaa za kiwanda hicho kukosa mtu wa kumlalamikia au kumuwajibisha pale itakapobainika kuwa bidhaa hizo hazijakidhi matarajio ya matumizi, mathalan kushika kutu mapema, kutoboka kwa wepesi, n.k.;
2. Bidhaa za kiwanda hicho zimekuwa zikiuzwa sokoni wakati bado hazijakaguliwa ubora wake na kuthibitishwa na Shirika la Viwango nchini (TBS).

Mabati 74 ya rangi ya kijani, 74 ya rangi nyekundu na 80 ya rangi ya bluu yalikutwa kiwandani hapo na uongozi wa kiwanda uliagizwa kutokuyauza mabati hayo. Aidha, sampuli mbili za mabati ya kiwanda cha Dragon Roofing Sheets zimewasilishwa katika maabara ya Shirika la Viwango Nchini (TBS) ili kuweza kubaini kama zinakidhi viwango vya uzalishaji wa mabati vilivyowekwa ka Shirika hilo kwa mujibu wa sheria au la;

Kwa upande wa kiwanda cha KAMAKA, Wakaguzi hawakupata bidhaa kiwandani hapo.

Aidha, Ukaguzi ulifanyika pia katika baadhi ya maduka ya vifaa vya ujenzi katika eneo la Buguruni ambapo pia sampuli moja ya bati zilizotiliwa shaka kukosa ubora iliwasilishwa TBS kwa ukaguzi wa viwango vya ubora vya zalishaji wa mabati.

Katika ukaguzi mwingine, tarehe 20 Februari, 2012, FCC kwa kushirikiana na wakaguzi wa "International Corporate Research-ICR" ilifanya ukaguzi wa bidhaa bandia za HP katika Mtaa wa Bridge, jijini Dar es Salaam. Katika ukaguzi huo FCC na ICR zilikamata jumla ya toner na catridges 43 zinazokadiriwa kuwa na thamani ya Sh. Milioni 6.35 katika duka lililopo jirani na Mgahawa wa Al Baasha.

Tume pia ilifanya kaguzi nyingine katika eneo la kariakoo tarehe 24 Januari na tarehe 1 Februari, 2013 ambapo ilikamata vipuri vya magari vilivyoghushiwa nembo ya biashara ya AK.

Kaguzi hizo zilizofanywa na FCC kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, zilitokana na malalamiko yaliyowasilishwa kwenye Tume na mmiliki wa nembo ya AK, kampuni ya Al Khair Auto Parts ya Dubai, Falme za Kiarabu.

Bidhaa zilizokamatwa katika ukaguzi wa Februari 1, 2013			
Na.	**Jina la Duka**	**Aina ya Bidhaa**	**Idadi**
1.	Several Auto Spare Parts, P.O.Box 7967, DSM	Disc Brake Pads Drum Brake Shoe	Seti 438 Seti 11
2.	Aisin Auto Parts, P.O.Box 7832, Dar es Salaam.	Brake Pads	Seti 738
3.	Nassor Chande Nassor	Brake Pads	23
JUMLA		Brake Pads Brake Shoe	Seti 1,199 Seti 11
Bidhaa zilizokamatwa katika ukaguzi wa Januari 24, 2013			
Jina la Duka		**Aina ya Bidhaa**	**Idadi**
BM Spare Parts		Disc Brake Pads	Seti 643
JUMLA KUU		Disc Brake Pads Brake shoe	Seti 1,842 Seti 11

Aidha, Tume ya Ushindani iliendesha zoezi lingine kubwa la ukaguzi wa kushitukiza tarehe 23 Novemba, 2012 katika eneo la Kariakoo baada ya kupata taarifa kutoka kwa Raia Mwema aliyearifu kuhusu kuwepo kwa maduka yanayouza vifaa bandia vya Umeme Nuru (Solar Panels) vyenye nembo ya EURO SOLAR.

Maduka mawili ya vifaa vya umeme nuru yanayomilikiwa na Bw. Charles Mwapashi yalikaguliwa na kukutwa yakiuza vifaa vya Umeme Nuru vilivyoshukiwa kuwa bandia

Katika ukaguzi huo, jumla ya Vifaa 176 vya Umeme Nuru (Solar Panels) vilikamatwa.

Kwa kipindi cha mwaka mmoja na nusu, kati ya Julai 1, 2011 na Desemba, 2012, Tume ilikamata jumla ya makontena 313 yakiwa na bidhaa mbalimbali bandia. Aidha, Tume ilifanya kaguzi 78 za kushitukiza katika mikoa mbalimbali nchini kwenye maduka na maghala ya bidhaa yaliyoshukiwa kuwa na bidhaa bandia na kuwaadhibu wafanyabiashara 272 kwa kujihusisha na biashara ya bidhaa bandia. Katika kipindi hicho bidhaa zenye thamani ya zaidi ya Sh 324,700,000 zilikamatwa.

WITO:

Serikali, kupitia vyombo vyake vya usimamizi wa ubora na uhalisia wa bidhaa/ulinzi wa haki-miliki ya utafiti ma ubunifu wa bidhaa (Intellectual Property Rights) pamoja na usimamizi wa mwenendo wa utendaji wa soko, imejizatiti kuhakikisha kuwa soko la Tanzania haligeuzwi kuwa jalala la bidhaa bandia na hafifu na hivyo wale wote wanaojihusisha na biashara ya bidhaa za aina hii, wafahamu kuwa siku zao zinahesabika.

Tume inapenda kuwaasa wananchi kununua bidhaa kutoka katika maduka yanayotambulika, hususan kwa wakala walioidhinishwa wa bidhaa husika na waepuke kununua bidhaa vichochoroni, mkononi au zilizotandazwa chini, kwa kuwa kwa kiasi kikubwa zinaweza kuwa bandia hasa kutokana na wauzaji wake kutokuwa na utayari wa kuwajibika kwa namna yoyote ile endapo mlaji aliyezinunua ataathiriwa nazo.

IMETOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO NA MAHUSIANO YA UMMA

Tume ya Ushindani
Ubungo Plaza, DSM
23 Februari, 2013